

Maswali

1. Watu wa Galilaya walikuwa wanaenda wapi?
2. Mbona walikuwa wanaenda Yerusakemu?
3. Yesu alikuwa amefanya nini kwa miaka mitatu?
4. Nini ingetendeka kwa hekalu iliyokuwa mlimani?
5. Walipokuwa wakikaribia Yerusalem, Yesu alituma wanafunzi wawili wafanye nini?
6. Mbona Yesu alitaka iwe hivyo?
7. Yesu alipokuwa kwa punda akienda Yerusalem, watu walitandaza nini wakipasa sauti?
8. Kikundi gani cha watu hakikupendezwa na kuingia kwa Yesu na shangwe?
9. Kuingia kwa shangwe kulikuwa na maana gani?

Majibu

1. Yerusalem.
2. Kwa siku kuu ya Pasaka.
3. Alisafiri, akafundisha na kuponya watu wengi.
4. Askari wa Warumi watabomoa ukuta jiwe kwa jiwe.
5. Waende kwa kijiji wafungue punda na mwana punda na wamletee
6. Haya yalifanyika ili maneno ya nabii Zekaria yatimie.
7. Watu walitandaza mavazi yao na matawi ya miti wakipasa sauti wakisema, "Hosana kwa Mwana wa Daudi."
8. Wakuu wa Makuhani hawakufurahia hayo makelele.
9. Kuingia kule kulikuwa mfano. Kulionyesha wakati mataifa watamkaribisha.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



43 Yesu anaingia Yerusalem

Marejeo

Mathayo 21: 1-11 na Luka 19: 28-44

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yesu alijitambulisha kama Mwana wa Mfalme wa Amani na vile watu walimkaribisha kwa vikelekele kama Masiya.

Maneno maalum

1. Yesu + umati + Yerusalem + Pasaka
2. Yesu + kuingia kwa mwisho + Yerusalem + miaka mitatu + ponya + marafiki +adui
3. Yesu ana huzuni + baadhi ya watu + kutosikiliza + ujumbe wa Mungu +haribu Yerusalem jiwe kwa jiwe.
4. Karibu na Yerusalem + wanafunzi wawili + punda + funga pamoja na mwana punda
5. Mwana punda + mavazi + matawi + barabara + kabla ya Yesu
6. Mwandamano ulikua + Hosana + wakuu wa makuhani
7. Yesu + mtulifu na mpole + kuingia na shangwe + kataliwa + mpango wa Mungu + mataifa yote + mkaribishe


43.1 Vikundi vya watu vilikuwa vinatoka Galilaya vinaelekea Yerusalemu kwa siku kuu ya Pasaka. Watu walikuwa na taharuki kubwa kwa ajili ya miujiza yenyen Yesu alifanya. Watu waliulizana maswali kama huyu Yesu ndiye nabii aliyetarajiwa kama Masiya.

43.2 Yesu alipotimia miaka 12 alikuja Yerusalemu kwa mara ya kwanza. Kwa sababu Yesu alijua kila kitu, alijua hii ilikuwa ni mara ya mwisho. Kwa miaka mitatu Yesu alikuwa amesafiri, amefundisha na kuponya watu wengi. Alikuwa ana marafiki wengi na maadui pia. Alijua ni hatari yeye kuenda Yerusalemu lakini alikuwa anatimiza matakwa ya Mungu.

43.3 Yesu alipoona hekalu kuu juu ya mlima, alilia. Aliangalia mji mkuu wa Mungu – watu walikataa kusikiliza ujumbe wa Mungu kwa hivyo Yerusalemu itaharibiwa. Askari wa Warumi wataharibu ukuta wa hekalu jiwe kwa jiwe.

43.4 Walipokaribia Yerusalemu, Yesu alituma wanafunzi wawili akawambia, “Enda kwa kijiji kinachowakabili, kule mtaona punda amefungwa pamoja na mwana punda. Wafungue na mniletee. Mtu akimuuliza kwamba mnafanya nini, mwambie, ‘mwalimu anawataka.’” Haya yalifanyika ndiyo maneno ya nabii Zekaria yatimiye: “...Tazama Mfalme wenu anamkujia, mpole naye amepanda punda mwana punda...”

43.5 Wanafunzi walienda na wakafanya vile waliambiwa. Walimletea punda na mwana punda na walikuwa wametandika mavazi yao juu. Wakati Yesu alikuwa ameketi juu ya mwana punda watu wengi walitandaza mavazi yao au matawi ya miti kwa barabara kama zulia.



43.6 Baadhi ya watu walienda mbele yake na wengine walifwata nyuma. Mwandamano uliendelea kukua, wanaume, wanawake hata watoto wote walipasa sauti na kuimba. Walipiga kelele wakisema, “Hosana, Mwana wa Daudi, ndiye Mbarikiwa, Yeye ajaye kwa jina la Bwana.” Kulikuwa na Kelele. Wageni waliuliza, “Ni nani huyu?” Waliwajibu kwamba, “Huyu ni Yesu wa Nazareti ya Galilaya. Ni Yule Mungu aliahidi kwamba, atakuja kupea watu uhuru.” Haya makelele yaliwakasirisha Wakuu wa Makuhani.



43.7 Yesu alikuja kama Mfalme si kama askari mwenye nguvu. Alikuwa mpole na mtulifu juu ya mwana punda. Yesu alikundua kwamba, “Kuingia kwake na Shangwe” ilikuwa ni mwanzo wa watawala kumkataa ingawaje ilikuwa kusudi la Mungu. Kuingia huku kulikuwa ni kionjo cha vile mataifa watamkaribisha tena wabarikiwe naye.